

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA SABA

KIKAO CHA AROBAINI

02 JUNI, 2017



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA SABA

KIKAO CHA AROBAINI– TAREHE 02 JUNI, 2017

I. DUA:

II. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

**322. MHESHIMIWA OMARY TEBWETA MGUMBA
(MOROGORO KUSINI MASHARIKI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Kuna vyanzo vingi mbadala vya maji katika Jimbo la Morogoro Kusini Mashariki kama vile Mto Mbezi, Mto Ruvu na chanzo cha maji katika Kijiji cha Bamba Kiloka:-

Je, Serikali ina mpango gani wa muda mfupi, kati na muda mrefu wa kutatua changamoto ya maji safi na salama katika Vijiji vya Mkuyuni, Madam, Luholole, Kibuko Mwalazi, Kibuko na Mfumbwe ikiwemo kupanua na kuongeza uwezo wa tanki la Mto Mbezi ili liweze kukidhi mahitaji ya sasa.

WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:

323. MHESHIMIWA DKT RAPHAEL MASUNGA CHEGENI (BUSEGA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:-

Je, Serikali haioni haja ya kurekebisha Road Licence au ifutwe ili ukusanyaji wa kodi hii uendane na matumizi halisi ya vyombo vya moto vya barabarani.

WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI:

324. MHESHIMIWA OMARY MOHAMED KIGUA (KILINDI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji:- Moja ya changamoto kubwa inayokabili maeneo mbalimbali nchini ni huduma ya maji safi na salama; Serikali kwa kushirikiana na Mashirika ya Kimataifa kama Benki ya Dunia wamekuwa wakitoa ahadi za kuwezesha miradi mikubwa ya maji nchini lakini mara nyingi wamekuwa hawatekelezi ahadi zao:-

Je, Serikali haioni sasa imefikia wakati wa kuweka mikakati ya dhati ya kutenga bajeti kwa kutumia mapato ya ndani ili kutoathiri miradi ya maji.

WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:

325. MHESHIMIWA JOEL MWAKA MAKANYAGA (CHILONWA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:- Wananchi wa Chilonwa wanaishukuru Serikali kwa kuendelea kukarabati daraja lililoko kati ya Kijiji cha Mahampha na Nzali kwa kiwango cha mkeka, daraja hili hupitisha maji mengi sana wakati wa masika toka Bwawa la Hombolo kiasi cha kukosa mawasiliano kabisa kati ya Kaskazini na Kusini mwa Jimbo na Wilaya ya Chamwino kwa ujumla wake:-

Je, Serikali ina mpango gani sasa wa kulijenga daraja hili kwa kiwango cha daraja la kupitika juu na sio mkeka ili kuondoa kero hii ya kukatika kwa mawasiliano kabisa wakati wa masika.

326. MHESHIMIWA SUBIRA KHAMIS MGALU (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:-

Je, ni lini ukarabati wa barabara ya Mlandizi - Chalinze utaanza kama ilivyoahidiwa katika Ilani ya CCM ya mwaka 2015.

WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:

**327. MHESHIMIWA CATHERINE VALENTINE
MAGIGE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:- Kwa zaidi ya miaka 21 sasa kumekuwepo na mkanganyiko katika ardhi ya Pori Tengefu la Loliondo hali ambayo inawatesa sana Wananchi:-

Je, Serikali itaondoa lini mkanganyiko huo.

**WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA,
WAZEE NA WATOTO:**

**328. MHESHIMIWA LUCY FIDELIS OWENYA
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:-

Je, moshi wa bangi una madhara gani kwa binadamu.

**329. MHESHIMIWA RAPHAEL JAPHARY MICHAEL
(MOSHI MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:- Hospitali ya KCMC inamilikiwa na Taasisi ya Kidini ikishirikiana na Serikali na imekuwa ikitoa huduma bora zinazofanya Wagonjwa wengi kutoka ndani na nje ya nchi kukimbilia Hospitali hiyo na hivyo kuifanya Hospitali hiyo izidiwe na uwezo wake wa kuhudumia Wagonjwa hususan miundombinu na samani za Hospitali:-

- (a) Je, Serikali ina mpango gani mahususi wa kuisaidia Hospitali hiyo ili iweze kutoa huduma bora zaidi kulingana na ongezeko kubwa la Wagonjwa wanaokwenda kutibiwa hapo;
- (b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza kiasi cha pesa inachopeleka katika Hospitali hiyo na kuhakikisha kuwa kile kiwango kilichotengwa kwa sasa kinapelekwa kwa wakati.

WIZARA YA NISHATI NA MADINI:

330. MHESHIMIWA MOHAMED OMARY MCHENGERWA (RUFJI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini:- Maeneo mengi ya Pwani huwa na madini mbalimbali:-

Je, eneo la Rufiji lina madini gani ili Wananchi hawa washauriwe ipasavyo kutouza maeneo yao.

III. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:

Kwamba, Bunge sasa likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati na Madini kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

(Majadiliano yanaendelea)

**DODOMA
02 JUNI, 2017**

**DKT. T. D. KASHILILAH
KATIBU WA BUNGE**